

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



MKUTANO WA NANE

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TANO

11 SEPTEMBER, 2017

MKUTANO WA NANE

KIKAO CHA TANO TAREHE 11 SEPTEMBER, 2017

I. DUA:

Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) alisoma Dua na kuongoza Bunge.

Makatibu mezani:

1. Ndugu Asia Minja
2. Ndugu Neema Msangi

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

- (1) Mhe. Dr. Mwakyembe (Waziri wa Habari, Sanaa na Michezo) – kny. Waziri wa Katiba na Sheria aliwasilisha Mezani:-

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba (Intergovernmental Agreement – IGA) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Bomba la la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (East Afrika Crude Oil Pipeline – EACOP) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania).

- (2) Mhe. Deo Ngalawa (Mwenyewe wa Kamati ya Nishati na Madini – aliwasilisha Mezani:-

Maoni ya Kamati ya Nishati na Madini kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba (Intergovernmental Agreement – IGA) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Bomba la la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (East Afrika Crude Oil Pipeline – EACOP) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania).

- (3) Mhe. Devotha Minja – Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Nishati na Madini aliwasilisha Mezani:-

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba (Intergovernmental Agreement – IGA) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Bomba la la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (East Afrika Crude Oil Pipeline – EACOP) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania).

III. MASWALI

OFISI YA WAZIRI MKUU

Swali Na. 53: Mhe. Dr. Raphael Masunga Chegeni

Nyongeza: Mhe. Dr. Raphael Masunga Chegeni
Mhe. Richard Philip Mbogo
Mhe. Kasuku Samson Bilago

OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

Swali Na. 53: Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa

Nyongeza: Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa
Mhe. Hamidu Hassan Bobali
Mhe. Salma Rashid Kikwete

Swali Na. 54: Mhe. Oran Manase Njeza (kny. Mhe. Hassan Pirmohamed)

Nyongeza: Mhe. Oran Manase Njeza
Mhe. Edward Franz Mwalongo

Mhe. Pascal Yohana Haonga
Mhe. Desderius John Mipata

Swali Na. 55: Mhe. Joseph Kizito Mhagama

Nyongeza: Mhe. Joseph Kizito Mhagama
Mhe. Anne Kilango Malecela
Mhe. Mbaraka Kitwana Dau

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Swali Na. 56: Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga

Nyongeza: Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga
Mhe. Kangi Alphaxard Lugola
Mhe. Hussein Mohamed Bashe

Swali Na. 57: Mhe. Dkt. David Mathayo David

Nyongeza: Mhe. Dkt. David Mathayo David
Mhe. Frank George Mwakajoka
Mhe. Shally Joseph Raymond

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

Swali Na. 58: Mhe. Maryam Salum Msabaha

Nyongeza: Mhe. Maryam Salum Msabaha
Mhe. Yussuf Salim Hussein

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

Swali Na. 59: Mhe. Alex Raphael Gashaza (kny. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka)

Nyongeza: Mhe. Alex Raphael Gashaza
Mhe. Martha Moses Mlata
Mhe. Lucia Michael Mlowe
Mhe. Flatei Gregory Massay

Swali Na. 60: Mhe. Dkt. Rashid Mohamed Chuachua

Nyongeza: Mhe. Dkt. Rashid Mohamed Chuachua
Mhe. Hassan Elias Masala
Mhe. Yahaya Omary Massare
Mhe. Catherine Nyakao Ruge
Mhe. Lucy Thomas Mayenga

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA
WATOTO**

Swali Na. 61: Mhe. Lucy Samwel Magereli

Nyongeza: Mhe. Lucy Samwel Magereli

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

Swali Na. 62: Mhe. Rose Cyprian Tweve

Nyongeza: Mhe. Rose Cyprian Tweve

WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI

Swali Na. 63: Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma

Nyongeza: Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Swali Na. 64: Mhe. Shabani Omary Shekilindi

Nyongeza: Mhe. Shabani Omary Shekilindi

Swali Na. 65: Mhe. Pauline Philip Gekul

Nyongeza: Mhe. Pauline Philip Gekul

WIZARA YA NISHATI NA MADINI

Swali Na. 66: Mhe. Abdallah Haji Ali

Nyongeza: Mhe. Abdallah Haji Ali

IV. MATANGAZO

- (1) Wageni 4 wa Mhe. Naibu Spika kutoka Umoja wa Mabunge Duniani – IPU.
 - Mhe. Winfred Masika – Uganda
 - Ndg. Hilary Gbedema – Geneva
 - Dkt. Sonia Palmieri – Australia
 - Ndg. Masheti Masinjila – Kenya
 - Ndg. Salome Anyoti
- (2) Mgeni wa Mhe. Japhery R. Michael – ambaye ni Mstahiki Meya Manispaa ya Moshi, Kilimanjaro.
- (3) Wageni 100 wa Mhe. Julius Kalanga Laizer ambao ni wanafunzi 90 na walimu 10 kutoka Mwalimu Anna English Medium Pre and Primary School, Arusha.

- (4) Wageni 40 wa Mhe. Zuberi Kuchauka ambao ni wanafunzi wa Liwale High School na Walimu wao kutoka Lindi.
- (5) Wanafunzi 80 na Walimu 3 kutoka Bwawani Secondary School, Morogoro.
- (6) Wageni wa Mhe. Maulid Mtulia kutoka Dar es Salaam wakiongozwa na Dkt. Jamal Katundu.

MATANGAZO MENGINE:

1. Mwenyekiti wa Bunge Sports Club – aliwatangazia Wabunge juu ya Matokeo ya Mpira wa Miguu uliofanyika tarehe 9/9/2017 ambapo Bunge Sports Club ilipigwa bao mbili kwa moja na timu ya Salasala ya Mhe Spika.
 - Pia Bunge Sports Club ilishinda timu ya Veteran bao 3 kwa 0 na mchezaji Nyota akiwa Mhe. Venance Mwamoto.
2. Mhe. Suzan Lyimo ameokota miwani na simu katika semina iliyofanyika Morena Hotel. Yeyote aliyepotelewa simu au miwani amwone Mhe. Mhe. Suzan Lyimo.
3. Taarifa ya Spika kuhusu Uongozi mpya ya Kambi ya Chama cha Wananchi (CUF) Bungeni kuwa tarehe 8/9/2017 Spika alipokea taarifa ya mabadiliko ya Viongozi wa CUF Bungeni kutoka kwa Kaimu Katibu Mkuu wa CUF – Mhe. Magdalena Sakaya na kuwa tarehe 6/9/2017 walichagua viongozi hao, ambao ni kama wafuata:-
 - Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma – Mwenyekiti
 - Mhe. Rukia Kassim Ahmed - Katibu
 - Mhe. Maulid Said Mtulia - Mnadhimu
 - Mhe. Sonia Jumaa Magogo - Mweka Hazina

MWONGOZO WA SPIKA

1. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, alisimama kwa kanuni ya 68 (7) kuomba Mwongozo kuhusiana na Wageni wanaokuja Bungeni kwa ajili ya mafunzo, ambapo wamekuwa wakicheleweshwa sana getini na kuingia Bungeni wakati Spika ameshaingia na maswali yameisha. Kwamba jambo hilo huondoa dhana nzima ya kuja kwenye mafunzo.

Naibu Spika alijibu:-

Hilo ni suala ambalo hushughulikiwa kiutawala. Hivyo Makatibu walichukue kuona namna nzuri ya kulirekebisha.

2. Mhe. Mbarouk Salim Ali, alisimama kuomba mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) kuhusu majibu yasiyoridhisha ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwamba mabenki hayakubali Hatimiliki za kimila na hivyo Wananchi wamekosa mikopo katika Mabenki, majibu ya Waziri alisisitiza vijana wajiunge pamoja kupata mikopo. Watapataje ikiwa Hatimiliki za Kimila haziruhusiwi.

Naibu Spika alijibu:-

- Kwanza Spika alishatoa Mwongozo kuwa anayepaswa kuleta malalamiko ya kutoridhika na majibu ni mwuliza swali la msingi hivyo swali hilo halijalalamikiwa na mwuliza swali.
 - Pia utaratibu wa mabenki haujatokea Bungeni.
3. Mhe. Hashim Jaku, alisimama kwa Kanuni ya 68(7) kuomba mwongozo kuhusu kauli ya Naibu Waziri wa Fedha alipokuwa akijibu swali Bungeni alisema Wabunge wamuunge mkono Mhe. Rais kitu ambacho kinaashiria kuwa wanaomuunga mkono Mhe. Rais ni Mawaziri tu, lakini walioko back bench hawamuungi mkono.

Mhe. Naibu Spika alijibu:-

Mhe. Naibu Waziri wa Fedha hakuwa na maana hiyo, bali alimaanisha twende pamoja katika jambo hilo.

Pia Mhe. Hashim Jaku aliendelea kuomba mwongozo kuwa Bunge lingetengeneza utaratibu ili Wabunge wapate nafasi ya kwenda kumtembelea Hospitalini Mhe. Tundu Lissu kumjulia hali.

Naibu Spika alijibu:-

Kwa kuwa huko Hospitali yupo Mhe. Freeman Mbowe na Mhe. Mchungaji Peter Msigwa, Bunge lisiwe na mashaka kwani taarifa za Mgonjwa zinapatikana na kupitia Waheshimiwa hao.

4. Mhe. Joseph K. Musukuma aliomba mwongozo kwa Kanuni ya 6(7) kuwa wakati Waziri wa Afya akitoa majibu ya nyongeza ya swali Na. 61 la Mhe. Magereli alitumia kauli moja ambayo imewaweka Wanaume katika hali sio nzuri kuwa Wanawake wahimize waume zao kupima UKIMWI ili wapate dawa Je, hata kama hawajaathirika wakapate dawa?
5. Mhe. Ally Saleh Ally aliomba mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) kuwa CUF inao uongozi wake na hivi karibuni wameshafanya marekebisho kujaza nafasi zilizoachwa wazi ili ifikishwe kwa Spika kwa taarifa, lakini inakjuwaje Chama kimoja kiwe na makundi mawili Bungeni? Je, kundi la wachache linaweza kufanya maamuzi kuliko kundi la wengi?

Naibu Spika alijibu:-

Chama cha Wananchi CUF kinaonesha kuwa na makundi mawili na moja limetoa taarifa na moja halijatoa hivyo, jambo hilo liko ndani ya Chama na siyo Bunge. Alishauri Chama hicho kiende kwa Spika ili kupata muafaka wa jambo hilo.

V. HOJA ZA SERIKALI

Azimio la Waziri wa Katiba na Sheria kuhusu Kuridhia Mkataba (Intergovernmental Agreement – IGA) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Bomba la la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (East Afrika Crude Oil Pipeline – EACOP) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania).

Uwasilishaji ji kama ifuatavyo:-

- (1) Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo (kny. Waziri wa Katiba na Sheria)
- (2) Mhe. Deo Ngawala (kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini.
- (3) Mhe. Devotha Minja – Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Nishati na Madini.

Uchangiaji wa Wabunge:-

- | | | |
|-----------------------------|---|-----|
| (1) Mussa Mbarouk | – | CUF |
| (2) Prof. Anna K. Tibaijuka | – | CCM |
| (3) Mhe. Juma Nkamia | – | CCM |
| (4) Mhe. Vedastus Manyinyi | - | CCM |

Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo (kny. Waziri wa Katiba na Sheria) alihitimisha hoja yake.

Naibu Spika kwa Kanuni ya 28 aliongeza dakika 30.

Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba (Intergovernmental Agreement – IGA) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Bomba la la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (East Afrika Crude Oil Pipeline – EACOP) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) liliridhiwa na Bunge.

VI. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 7.05 Mchana Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne tarehe 12/9/2017 saa tatu asubuhi.